



SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MOJA WA MWAKA WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba **Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja wa Mwaka wa Wanahisa** wa Kampuni ya Soko la Hisa la Dar Es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange PLC - DSE) utakaofanyika katika **Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo - Exchange Tower, NHC Morocco Square, Kiwanja 1-3/44, Barabara ya Mwai Kibaki / Mtaa wa Ursino**, Dar Es Salaam na pia kwa njia ya mtandao kupitia **eAGM Mkutano Platform**, siku ya **Ijumaa tarehe 12 Juni 2026** kuanzia **saa tatu na nusu asubuhi** (9.30 a.m.) kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kufungua Mkutano;
2. Kupitisha Ajenda ya Mkutano;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi wa Mwaka;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi wa Mwaka;
5. Kupokea na kupitisha
 - 5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa Mwaka uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2025;
 - 5.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya DSE na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2025;
 - 5.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya *Fidelity Fund* na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2025;
6. Kuidhinisha Pendekezo la Malipo ya Gawio kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2025;
7. Kupitisha Malipo ya Wakaguzi wa Nje;
8. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa Mwaka wa Fedha 2026;
9. Kuidhinisha Malipo ya Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026; na
10. Mengineyo.

Maelezo:

- (i) Wanahisa watakaotaka kushiriki katika Mkutano kwa njia ya mtandao, wanatakiwa kutoa taarifa kwa Mwanasheria wa Kampuni kwa njia ya simu na.. +255746160516 / +255677070414 au kwa barua pepe kupitia info@dse.co.tz or registrar@cldr.co.tz kuanzia tarehe 5 Juni 2026 ili kupatiwa kiunganishi cha Mkutano huo;
- (ii) Mwanahisa atakaye hudhuria Mkutano kwenye Ukumbi atatakiwa kufika na namba yake ya akaunti ya hisa "CDS Account Number" pamoja na kitambulisho chake.
- (iii) Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanahisa ni taasisi/kampuni, mwakilishi anatakiwa kuwa na fomu za uwakilishi ziwe zimegongwa muhuri wa kampuni. Fomu hizo zifikishwe kwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi katika ofisi za DSE kabla ya saa nane mchana (02:00 p.m.) tarehe 11 Juni 2026.
- (iv) Mwanahisa anaweza kumteua Dalali wa Soko, mmoja wa Wakurugenzi wa DSE (Non-Executive Director), au Msajili wa Hisa (CSD & Registry Co. Ltd) kama mwakilishi. Wanahisa wanahamasishwa kutumia wawakilishi na wanashauriwa kuteua wawakilishi kwa kujaza fomu za uwakilishi.
- (v) Vitabu vyenye taarifa za hesabu kwa mwaka 2025 pamoja na fomu ya mwakilishi vitapatikana katika Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo la Exchange Tower, Barabara ya Mwai Kibaki / Mtaa wa Ursino na kwa Madalali wa Soko la Hisa la Dar es Salaam kuanzia tarehe 5 Juni 2026.
- (vi) Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa tarehe 9 Juni 2026.

Kwa Agizo la Bodi

Mary Stephen Mniwasa
Katibu wa Bodi
14 Mei 2026